

KWA IMANI, MUSA

 Asante, Ndugu Neville. Habari za asubuhi, jamani. Ni vema kuwa hapa leo maskanini. Nami niliwazia labda kama nilimfanya Ndugu Neville kuzungumza asubuhi ya leo, ningejaribu usiku wa leo. Halafu basi nilikuwa nikirejea nyuma basi kwenye somo moja la shule ya Jumapili kwa ajili ya asubuhi ya leo. Na ninii... Bwana akipenda, tutajaribu ku—kuwa na somo hili la shule ya Jumapili.

² Sasa, imekuwa majuma mawili sasa, yapata, tangu nilipoingia. Nami nimekuwa na wasiwasi sana kama mlivyofahamu, ya kwamba, huko hudumani, nilichoka sana sana, wala nisingeweza kuendelea zaidi. Ndipo basi ikanibidi kurudi kwa mapumziko kidogo tu. Nami nilichukua kama siku tatu huko Wolf Creek Dam, huko chini Kentucky, mahali nilipozaliwa. Nikawazia, “Loo, ninajisikia vizuri sana sasa. Niko sawa.”

³ Basi nikarudi nyumbani, na jambo la kwanza kunikabili usoni lilikuwa ni namna fulani ya jambo la kiserikali pamoja na kodi ya mapato. Nilishuka mpaka chini kabisa tena. Kwa hiyo nikatambua itachukua zaidi ya juma moja ama mawili kupumzika kabisa.

⁴ Nayo huduma yangu iko karibu kubadilika sasa. Na sina mikutano iliyopangwa. Na hiyo ndiyo sababu kwa namna fulani nilikuja tu kando, na nikawaza, na sasa kwa majuma machache yajayo, nitapumzika tu, mapumziko kamili, na kumngojea Bwana.

⁵ Na wengi wenu ninyi watu hapa ndani, ambao ni watu wa zamani, ambao mmekuwa nasi kwa muda mrefu sana, mnakumbuka ya kwamba kile Bwana ametwambia, Yeye sikuzote amefanya yale aliyosema angefanya.

⁶ Kumbukeni, wakati hapo mwanzoni kabisa, kanisani hapa, ile asubuhi tuliyouweka lile jiwe la maskani, jinsi ambavyo Yeye... Imeandikwa, na iko kwenye jiwe, kwenye ule ukurasa mtupu wa Biblia yangu. Asubuhi hiyo, lile ono kuu, lilisema, “Hii siyo maskani yako.”

⁷ Nilisema, “Iko wapi, Bwana?” Akaniweka nje chini ya anga. Ndipo Sauti ikaja. Nami nikaangalia nikaona misalaba mitatu, kitu kama hicho, miti na tunda lao, kadhalika. Mnajua kile hilo ono lilicho. Limeandikwa, kwa miaka kadha.

⁸ Wakati nikikichukua, hivi majuzi, kitabu cha zamani kule juu, nikisoma baadhi ya mambo ambayo Bwana alikuwa ameyasema, yaliyotabiriwa; tayari yametukia. Juu ya upuuzi

huu wa vijana, na kuhusu jinsi ambavyo vita vingetokea, na mambo hayo yote yametimia.

⁹ Mambo mawili tu yamesalia, katika moja ya unabii huo mkuu. Hayo ni, kwamba magari yawe barabarani yenye kitenzambali, yakionekana kama yai, ila tu huliendesha. Linajiendesha lenyewe. Kisha kutakuwako na mwanamke mashuhuri atakayeinuka, maana Marekani ni taifa la mwanamke. Nalo litaninii. . . Mwanamke mashuhuri atainuka, na kuwa Rais ama kitu kama hicho, katika taifa hili. Ndipo kutatokea maangamizi kamili. Taifa lote litaangamizwa.

¹⁰ Na, kwamba, ninabashiri. . . Sasa hili si Bwana anayelisema hili. (Hilo lingine, kuhusu mwanamke, ndilo, ni Bwana.) Lakini nilibashiri, katika mwaka wa 1933, ya kwamba ulimwengu ungeyafikia maangamizi kamili kabla ya mwaka wa '77.

¹¹ Kwa hiyo, sikujua wakati huo ya kwamba walikuwa na kitu ambacho kingeweza kuuangamiza kama walivyo nacho sasa, bali nililionga hili taifa katika maangamizi kamili, visiki tu vya miti na vitu kama hivyo, vimesalia.

¹² Kwa hiyo, yanakuja. Na kama mambo haya mengine yote yametimia kama vile tu Yeye alivyosema, hilo pia litakuwa, ni kama tu vile Yeye alivyosema katika Maandiko hapa, yale Yeye asemayo, iwapo Kristo alikuja mara ya kwanza, Yeye atakuja mara ya pili. Na mambo yote alivyosema yatatimia. Basi tukiliona hili barabara, na tukijua ya kwamba sisi ni. . . namba yetu iko karibu kabisa kuitwa, kama taifa, tukijua ya kwamba Kanisa liko karibu na Kunyakuliwa Kwake. Inausisimua moyo wa mhudumu, ama mshirika yeyote, kujua ya kwamba tuko katika siku hii na wakati tunamoishi. Ndio wakati ulio mkuu zaidi ambao mtu yeyote aliwahi kuishi duniani, ni sasa hivi; hiyo ni kusema, kwa ajili ya Kanisa. Kwa hiyo, hakika ninayatamani maombi yenu.

¹³ Ndipo basi nikaona humu maskanini, na nikaona kwamba walikuwa. . . watakuwa na marudio fulani ya uchaguzi na kila kitu, kanisani, kwa baadhi ya halmashauri na kadhalika.

¹⁴ Na—nalo kanisa lilihitaji mkutano mdogo, kuchochewa kidogo. Nanyi sikuzote mmekuwa wema kwangu, na kunibariki. Na mimi kuwa mahali hapa, inaonekana ilikuwa ni baraka kwenu. Nami nina hakika, kuwa pamoja nanyi, kumekuwa ni baraka kwangu. Nanyi sikuzote mmekubali yale nilivyosema kwamba ni Kweli, jinsi nilivyoliona kwa njia ya Mungu. Nami na—nathamini hilo.

¹⁵ Kwa hiyo basi, nilianza kuja, kisha ilikuwa nitafute kujua, na kulinyosha kanisa letu, katika halmashauri zake, halafu kwa ajili ya uchaguzi na kadhalika. Ndipo basi—basi, niliwazia, baada ya hilo, nilitoka nikapumzika kidogo kabla sijarudi hudumani tena.

¹⁶ Liwekeni miongoni mweni. Sasa, si kwa ajili ya watu wa nje. Ni kwa ajili ya maskani hii. Tunataka mkutano na maskani hii, kusudi kila kitu, na kila kosa, mambo yote ambayo yamekuwa yakiendelea, na labda hisia ndogondogo mmoja kwa mwingine; hao, nitamchukua kila mmoja wao na kuwaleta uso kwa uso kabisa. Kwa hiyo kama hutaki kukabiliana na hilo, afadhali uondoke nchini; maana utakabiliana uso kwa uso na kila moja ya hayo, kama tulivyozea kufanya hapa maskanini. Na yote yatanyoshwa, kwa sababu sisi ni ndugu na dada ambao tumemea ushirika, ule Mwili wa Kristo, kwenye meza ya baraka. Wala si kitu ila ni ibilisi ambaye angefanya chochote ambacho ni kibaya, na angesababisa hisia, ama kurarua, ama chochote kama hicho. Nami ninamchukua Ndugu yetu Neville, nasi tutaenda mahali hadi mahali, na kuwaleta watu kwa watu, pamoja, mpaka ile maskani ya kale irudi, imeimarishwa tena, imesimama, ipate kuendelea kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Sasa, hii ni, sababu ya kusema jambo hili, ni kwa sababu liko na kundi letu dogo hapa asubuhi ya leo.

¹⁷ Na sasa naenda kupumzika kidogo, halafu nirudi upesi niwezavyo. Kisha ninatarajia kuondoka kwenda hudumani tena. Ndipo wakati huu, Bwana akipenda, ninataka kuchukua kile kidogo ambacho tumekusanya kwa njia ya fedha, na kadhalika, yangu mwenyewe, huko nje kwenye. . . mpango huu wa umishenari wa nchi za kigeni. Nami nijinunulie hema jipya, na vifaa vipya, niingie hudumani. Sio kanisa hadi kanisa, bali kwenda kwenye mikutano yetu wenyewe.

¹⁸ Sasa, siyo kuwadharau ndugu ambao wamenialika, ambalo ni zuri sana. Lakini zaidi sana, unakuta mikutano hii mikubwa, wao husema utakuwa kule, ndipo basi marafiki wako wote wanakuja, na halafu kuna kupiga debe kwingi kwa ajili ya pesa. Linawafilisi hao watu sana. Ndio kwanza nianze kuliona jambo hilo, mnaona. Kwa hiyo hilo—hilo si sahihi. Tunataka kuwa na mahali ambapo tunaweza kuwaleta. Si lazima ulete pesa zako. Njoo tu, wewe mwenyewe, na—na kumtumikia Bwana. Unaona? Na kwa hiyo sasa. . .

¹⁹ Nayo huduma yangu imebadilika sasa hivi. Mnakumbuka wakati nilipokuwa nikishika mkono wa mtu, na kusimama tu hapo, naye Bwana angeniambia mimi shida ilikuwa ni gani. Kasema, “Basi itakuwa, utajua siri ya moyo wa watu.” Kila mmoja wenu anajua hilo limetukia kikamilifu kabisa jinsi alivyosema. Sasa hii ndiyo hatua inayofuata, ambayo imetabiriwa na kubashiriwa, ambayo itakuwa iko juu sana kuliko nyingine yoyote, mnaona. Nayo sasa hivi inabadilika.

²⁰ Na hiyo ndiyo sababu Shetani ananishambulia kwa kodi ya mapato, akijaribu kuniambia, serikali, ya kwamba ninadaiwa kodi ya mapato kwenye kila senti niliyopata, kama mhudumu, tangu miaka ishirini na saba iliyopita, nilipoingia hudumani. Sivyoyote, maana zilipitia kwenye kanisa hapa.

21 Mimi ni mdhamini wa kanisa hili. Hiyo ni kweli kabisa. Liko kwenye kumbukumbu hapa. Kwa hiyo, basi, kama mimi ni mdhamini-mweka hazina wa kanisa hili, basi hakuna kitu ulimwenguni...Serikali haina uhusiano wowote nalo. Hawalihoji kanisa. Wananihoji mimi nikiwa ni mweka hazina wa kanisa. Nao wadhamini wametia sahihi karatasi iliyo kwenye benki huko, ya kwamba fedha zangu zote...Badala ya kuwa na wakfu wangu mwenyewe, nilizipitisha kwenye kanisa langu hapa, maana bila shaka ni wakfu, kwa vyovyote vile.

22 Na kufanya hivyo, hunisaidia kutolitoroka kanisa na kuliacha, na kuendelea huko nje na pasipo kuwepo kitu chochote hapa. Baada ya mimi kuwaahidi watu kwamba ningerudi kanisani, wakati baada ya wakati, na kuwasaidia. Hiyo ndiyo sababu nililiweka jinsi hii, kwa sababu niliwaahidi ninyi watu. Hiyo ndiyo sababu ninakaa nalo namna hiyo, badala ya kuwa na mtu binafsi. Ndipo, kama ukifanya hivyo, inalitupilia kwenye dhehebu. Nami ninalipinga dhehebu kwa dhati. Kwa hiyo ni—nitalidumisha jinsi tu lilivyo, mikononi mwa Mungu, ili tuweze kusonga mbele kwa ajili ya Ufalme wa Mungu.

23 Sasa, asubuhi ya leo, tunataka kulisoma Neno hili la kale lililobarikiwa, na kuamini.

24 Sasa, nataka kusema, pia...Ninamwona Ndugu Egan na wengi, baadhi ya wadhamini wameketi hapa, baada ya kufanya mkutano wetu wa wadhamini, hivi majuzi usiku; ni kweli, nilitangaza hadharani mbele ya kanisa, ya kwamba kila mmoja wenu nyote si wadhamini wa—walioteuliwa tena. Nyinyi ni wadhamini waliochaguliwa, nalo jina lenu liko kwenye vitabu. Vema.

25 Na sasa watafanya uchaguzi mwingine wa—wa mashemasi, na kadhalika. Naye Ndugu Neville ni, atawaita hao mara baada ya ibada hii, vema, na kwa ajili ya mweka hazina na kadhalika, tunapoliweka sawa kanisa. Kuifanya, misingi yote, tayari, ndipo tunaweza kuwa na uamsho unapokuja.

26 Sasa, kabla tu hatujazirudia kurasa hizi hapa, kwa ajili ya somo letu la shule ya Jumapili, kwenye Neno hili kuu la Mungu aliye hai, hebu na tuviinamishe tu vichwa vyetu, dakika chache, tunaponena na Mwandishi wa Kitabu hiki. Na sasa tuweke kando kila wazo, kila kitu kilicho kinyume, kuwafanya msiwe na baraka.

Na tuombe.

27 Mungu aliye mtakatifu sana na wa haki, katika Uwepo Wako adhimu tunakuja sasa, tukikutolea Wewe maisha yetu, na nafsi ze—zetu, na miili yetu, na ibada zetu, na vipaji vyetu. Na yote tuliyo nayo, tunayakabidhi Kwako. Basi unapotuangualia sisi, Bwana, kukiweko na dhambi yoyote dhahiri na isiyoundamwa, tungekuomba Wewe, Ee Bwana Mungu, ya kwamba Wewe utaitumia Damu ya Mwana Wako, Yesu, mahali kama hapo. Kwa

kuwa, tukitambua ya kwamba sisi peke yetu hatujitoshelezi, na hapo haiwezekani sisi kujikimu wenyewe. Bali tunategemea kabisa Damu Yake ya thamani, na neema Yake kutumiwa mahali petu, kusudi sisi wenye dhambi tusiostahili tuweze kuja kwa ujasiri siku moja Mbele Zako, tukileta mbele zetu Damu hii ya Bwana Yesu. Ambayo, Wewe, katika nyakati zilizopita, umeitambua kuwa ni Damu ya Mwana Wako wa pekee, na umefanya ahadi, kwamba, “Kupitia Yeye, kama tukizikiri dhambi zetu, tutahesabiwa haki kwa neema Yake.”

²⁸ Na sasa tungeomba, Bwana, ya kwamba Wewe utatusamehe kosa lolote, dhambi yoyote ya makosa ama ya kuachilia, makosa, kwamba kama wazo lolote ovu limeichoma nafsi yetu, kwa mishale yenye moto ya ibilisi, kwamba Wewe utaondolea mbali huyu adui Wako mwovu, na wa watu Wako.

²⁹ Nasi tungeomba ya kwamba Wewe utamtuma Roho Mtakatifu alishike Neno kwenye wakati huu, tunapojitolea kama vyombo, kwamba unene kupitia sisi, na kusikia kupitia sisi, Neno Lako. Na ujalie sisi nasi tulipokee kama kutoka Kwako, na kuondoka mahali hapa, leo hii, tukijisikia ya kwamba tumewekwa sawa tena kwa huduma ya Kristo; tupate kustahili vema zaidi kwa ajili ya ibada ya usiku wa leo na kesho, kwa sababu ya kuzuriwa na Roho Mtakatifu.

³⁰ Wabariki ndugu zetu kila mahali, makanisa kote ulimwenguni, ambayo yanalishikilia Neno la Uzima katika siku hii ovu. Tunajisikia kwamba hakuna wakati mwingi uliosalia wa kufanya kazi, kwa kuwa usiku unaingia upesi. Mawingu ya vita yanaelea tena. Uovu umekaribia, nasi tunaomba ya kwamba Wewe utaturuhusu tufanye kazi kuliko hapo awali. Pumzisha miili yetu iliyochoka, Bwana, na ututume turudi vitani. Kwa kuwa tunaomba katika Jina la Bwana Yesu, na kwa ajili Yake tunaomba. Amina.

³¹ Tunapofungua, asubuhi ya leo, Biblia, kwenye m—mlango wa 11 wa Kitabu cha Waebrania.

³² Jumatano usiku tulikuwa tukizungumza juu ya mlango wa 7 wa Kitabu cha Waebrania, juu ya “Melkizedeki, akiwa bila baba, na bila mama, bila mwanzo wa siku zake, wala mwisho wa maisha.”

³³ Nami nikawazia, labda, asubuhi ya leo, ingefaa kufungua tena Kitabu hiki cha ajabu, kwa kuwa tunayo misingi ya yale tunayotaka kusema, katika masomo ya hapo awali. Basi tukiruka mlango wa 10, na mlango wa 9, ambao ni sheria za kutoa dhabihu, tungefikia mahali pa “imani.” Basi hapa katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 11, na kuanzia kifungu cha 23, tunasoma hivi:

Kwa imani Musa, alipozaliwa, akafichwa miezi mitatu na wazazi wake, kwa sababu waliona ni mtoto mzuri; Wala hawakuigopa amri ya mfalme.

Kwa imani Musa alipokuwa mtu mzima, akakataa kuitwa mwana wa binti Farao;

Akaona ni afadhali kupata mateso pamoja na watu wa Mungu, kuliko kujifurahisha katika dhambi kwa kitambo;

Akikesabu ya kuwa kushutumiwa kwake Kristo ni utajiri mkuu kuliko hazina za Misri: . . . na kwa kuwa aliyatarajia hayo malipo.

Kwa imani akatoka Misri, asiogope ghadhabu ya mfalme: maana alistahimili kama amwonaye yeye asiyeweza kuonekana.

³⁴ Ninataka kuchukua somo, asubuhi ya leo, “kuchagua kwa imani.” Nami nataka kuchukua kwa ajili ya somo, hayo maneno matatu ya kwanza ya mlango wa 23, *Kwa Imani, Musa*. Basi, “kuchagua kwa imani,” karibu kila kitu tunachofanya, inatubidi kuchagua kwa imani. Na yote tunayoona ya kwamba Musa alifanya, yanayostahili kurudiwa, yalikuwa ni kwa imani; sio kwa kutazama, bali kwa imani.

³⁵ Na sababu ya mimi kulichagua hili asubuhi ya leo, kwa kanisa katika hali hii, imekuwa kwamba katika ninii zetu . . . hata shule zetu, na kote kote, tumekuwa na mafundisho mengi sana ya kisayansi. Kwa sababu ya jambo hili, tumewaondoa watu kwenye imani. Sasa, imani haithibitishwi na sayansi. Imani ni kile sayansi haioni. Nasi . . . kama kamwe tukiipoteza imani hii kuu, basi tuko gizani kabisa, hiyo . . . haidhuru tumeelimishwa vizuri jinsi gani, jinsi tungeweza kulielezea Neno la Mungu, kuistahilisha njia yetu ya kuamini.

³⁶ Kamwe hakuna njia ya kumfurahisha Mungu, ila kwa imani. Maandiko yanaliweka waziwazi hivyo, na ni kwa imani. “Basi pasipo imani,” Maandiko yanasema, “haiwezekani kumpendeza Mungu.”

³⁷ Kwa hiyo, kama imani isipokubaliana na sayansi, nayo sayansi isikubaliane na imani, hiyo inazifanya ku—kupingana zenyewe, basi inatubidi kufanya chaguo kama Musa alivyofanya. Kwa imani tunaamini!

³⁸ Sasa, kama tukiipoteza imani, basi maombi yetu kamwe hayatajibiwa na Mungu. “Kwa kuwa yeye amjiaye Mungu hana budi kwanza kuamini kwamba Yeye yupo, na huwapa thawabu hao wamtafutao kwa bidii.” Kwa hiyo, kama tukiipoteza imani, maombi yetu yanabatilika; hatufiki popote.

³⁹ Kwa hiyo ndiyo tu tunayoweza kuwazia, asubuhi ya leo, ni kuishikilia imani. Ndipo, kama tukiipoteza imani, matumaini yetu yote yamepotea. Na kama tukiipoteza imani, uhalisi wetu wote wa kiroho umepotea. Kwa kuwa, huwezi kuwa na imani katika mambo uyaonayo, kwa kuwa mambo uyaonayo yote ni ya kuharibika.

40 Kama tukimwangalia mtu fulani mashuhuri, mhudumu mashuhuri, ama kusanyiko kubwa, wote wataangamia, siku moja. Na kama tukiliangalia taifa kuu, ama silaha kuu, zote zitaangamia, siku moja. Ndipo basi hatuna budi kuishi kwa imani, juu ya mambo hayo ambayo sayansi haitangazi. Ni kwa imani tunaamini.

41 Sasa, tunapoteza utukufu wetu kama tukipoteza imani. Sasa, tukiondokea imani, basi tunalipeleka kanisa kwenye milki ya kiakili.

42 Na mara nyingi, imewaziwa, miongoni mwa watu, ya kwamba kwa sababu kusanyiko lilikuwa kubwa, nao walikuwa na makanisa makubwa, minara mirefu, na watu mashuhuri, waliovalia vizuri na kunadhifika, na fedha nyingi, hata wangeweza kumudu vitu kama hivyo, sisi, mara nyingi, tulidhani hilo lilikuwa linaleta uvuvio, kwamba kanisa fulani hili hapana budi limevuviwa. Ama, mara nyingi tumerejea kwa wahudumu mbalimbali ambao hutoka wakaenda hudumani na kuwa na umati mkubwa, nasi tunafikiri, wakati mwingine, ya kwamba hizo ni ishara za uvuvio. Lakini kwa jumla hiyo si kweli. Huo ni uvuvio wa kibinadamu.

43 Lakini uvuvio halisi huja kwa kuyatenda mapenzi ya Mungu. Mnaona? Iwe ni mmoja, ama watu wachache tu. Kama ni kanisa kubwa, ama kanisa dogo, haijalishi. Kama ni mnenaji mkuu, mwenye ufasaha wa lugha, ama mtu ambaye karibu hazijui ABC zake, haijalishi. Inategemea ujumbe anaoleta, kama umevuviwa na Neno la Mungu, ama, umevuviwa na dhana za kiakili za uvuvio wa kibinadamu?

44 Baadhi ya watu wanaweza kuvuviwa kwa sababu ya mnenaji mwenye ufasaha wa lugha. Hilo halilifanyi sahihi. Wakati mwingine wanavuviwa kwa sababu mtu huyo amefunzwa vizuri sana hata angeweza kuelezea hoja yake. Hiyo haimaanishi kwamba ni ya Mungu. Mnaona?

45 Ni kupitia kwa Neno la Mungu lililobarikiwa, lisilo na mwisho, la Milele pekee, tunaweza kupokea uvuvio, na huo unatolewa na Roho Mtakatifu. Kwa imani tunaupokea.

46 Sasa tungeweza kuwazia juu ya Musa, na wakati huu mkuu wa maisha yake. Nasi tusome, juu ya kuzaliwa kwake, na jinsi ambavyo Mungu alikuwa amemshughulikia, lakini ilifika wakati katika maisha ya Musa ambapo ilibidi kuweko na wakati wa kuchagua. Kama tukisoma vizuri, tunaona ya kwamba yeye alikuwa ni mwana wa binti ya Farao, naye alikuwa mrithi wa kiti cha enzi, naye angaliweza kuwa farao anayefuata katika Misri. Kwa hiyo yeye angalionwa wakati akitazama kote, akiisha kuwa mtu mzima na wa kuwajibika, nako kungekuwako na hao watumwa kwenye mashimo ya maji yaliyotuma. Naye Musa, wakati alipoangalia kupitia dirisha la ikulu, juu ya watumwa

wale wale ambao Farao aliwaangalia, bali ilikuwa ni tofauti jinsi gani katika kule kuangalia.

⁴⁷ Ninataka kuliwekea msingi wazo hilo, asubuhi ya leo, kwa dakika chache, na Mungu wa Mbinguni alishindilie kwenye kila moyo hapa. Ni jinsi unavyoangalia kitu chochote, ndiyo inayoleta tofauti.

⁴⁸ Yule mwinjilisti mashuhuri, John Sproul, ambaye alikuwa ni mwongofu wa huduma ya Ndugu Bosworth, ambaye wengi wenu mnamkumbuka miaka kadhaa iliyopita, wa lile Banda la Kale la Utukufu. Yeye alisema, siku moja alikuwa akifanya ziara, kabla ya kuaga dunia kwa mwenzake mpendwa tena mke. Walikuwa huko La Salle, Lorraine, Ufaransa. Nami nilikuwa na majaliwa ya kupatembelea mahali papo hapo. Naye yule kiongozi alikuwa akiwatembeza bustanini, na kuwaonyesha mambo mbalimbali. Ndipo wakaifikia sanamu fulani ya Bwana Yesu, kule kusulubiwa. Basi Bw. Sproul alikuwa amesimama kwa mbali, akiangalia, yeye pamoja na mkewe, ndipo, mioyoni mwao, walikuwa wakikosoa kile huyo mwanasanaa hapana shaka alikuwa nacho niani, ama huyo mchongaji, hasa, wakati alipochonga kutoka kwa jiwe, kitu kinachoonekana cha kuchukiza sana kuwakilisha mateso na upendo na huruma za Bwana Yesu, na jinsi yote ilivyoonekana kuchongachongwa ovyo ovyo. Ndipo kiongozi akamjia Bw. Sproul, akasema, “Bwana, nadhani unaikosoa sanamu hii ya Bwana Yesu.”

Naye akasema, “Ninaikosoa.”

⁴⁹ Akasema, “Sijashangazwa hata kidogo, kwa sababu watu wengi wanaoiangalia hiyo, kwanza, huwa wanaikosoa.”

⁵⁰ Ndipo Bw. Sproul akasema, “Mbona, siwezi kuona huzuni yoyote wala uvuvio wowote kwa kukiangalia kitu kama hicho, kwa hiyo ninashangaa ni kwa nini huyo mchongaji kamwe alikitengeza namna hii.”

⁵¹ “Naye huyo mchongaji. . .” Kasema, “Bw. Sproul, sanamu hii iko sawa kabisa, naye mchongaji alikuwa na jambo sahihi niani mwake. Ila palipo na shida, unayo wewe. Ni jinsi unavyoiangalia.” Ndipo akamshika mkono yeye pamoja na mkewe, akawashusha penye madhabahu chini ya msalaba huu unaotajwa. Naye akasema, “Sasa, Bw. Sproul, tazama juu sasa.” Ndipo alipotazama juu, alisema moyo wake nusura uzimie. Ni tofauti jinsi gani iliyokuwapo, kusimama huko kando na kuiangalia namna *hiyo*, na kushuka na kuiangalia jinsi ilivyokuwa imetengenezwa kuangaliwa.

⁵² Na hivyo ndivyo Mungu alivyo. Hivyo ndivyo imani ilivyo. Ni jinsi unavyoiangalia. Ukiangalia kama namna fulani ya Biblia ya kihistoria, ya kitu fulani kilichokuwa kwenye siku zilizopita, kamwe hutaweza kupata thamani halisi ya Biblia. Unapaswa kupiga magoti, na kuzitii amri za Biblia hii, na kuiangalia kupitia macho ya Roho Mtakatifu.

⁵³ Ningeliuliza kusanyiko hili, asubuhi ya leo. Mungu wa kihistoria anatufaa nini leo kama Yeye si Mungu yule yule? Anafaa nini Mungu, ambaye angemchukua Musa na kufanya miujiza aliyofanya naye, ingetufaa nini kusoma habari za Mungu kama huyo ikiwa Yeye si Yule yule leo? Anafaa nini Mungu ambaye angewakomboa kutoka kwenye tanuru la moto, wale wana wa Kiebrania, ikiwa Yeye si Mungu yule yule leo hii? Anafaa nini Mungu ambaye angehukumu kati ya mema na mabaya, katika siku zilizopita, na kuadhibu wenye makosa na kubariki wenye haki, kama Yeye si Mungu yeye yule leo hii? Tunaenda kanisani kwa sababu gani? Kwa nini tunayaacha mambo ya ulimwengu, kama Yeye si Mungu yule yule wa hukumu ile ile, na maoni yale yale aliyokuwa nayo sikuzote? Ingekuwa na faida gani kwa Mungu ambaye angeweza kuugusa mkono wa mwanamke mwenye homa kali, nayo hiyo homa iishe, iwapo Yeye si Mungu yule yule leo hii? Ingekuwa na faida gani kumtumikia Mungu ambaye angemwita rafiki Yake kutoka kaburini, baada ya kufa siku nne, endapo si Mungu yeye yule leo hii?

⁵⁴ Kwa imani tunaamini ya kwamba siku fulani yenye utukufu Yeye atatuia kutoka duniani, japo tuwe ni kijiko cha mavumbi tena. Tunathibitishaje hilo? Hatulithibitishi. Tunaliamini. Hatujaombwa kuthibitisha chochote. Tumeombwa kuliamini.

⁵⁵ Kwa imani Musa alifanya *hili-na-lile*. Na kama vile Musa, akiwa kijana mwanamume, alivyowaangalia hao watumwa, kupitia kwenye dirisha la ikulu, akaona kundi lile lile la watumwa wenye taka, wachafu, waliojaa matope ambao Farao aliwaona.

⁵⁶ Naye Farao alipowaangalia, na Wamisri, hawakuwa kitu ila kundi la watumwa. Hilo ndilo tu walilojua; kuwa tu wanadamu wakanyaga matope, kutengeneza matofali ya matope kwa ajili ya miji ambayo Farao alikuwa akijijenga. Hivyo ndivyo Wamisri na Farao walivyowaangalia hao watumwa.

⁵⁷ Lakini Musa, wakati alipowaangalia, ulikuwa ni mtazamo tofauti alikuwa nao Musa. Wakati alipoona, huku wakipita karibu na dirisha, makunyanzi makubwa usoni mwao, machozi yaliyotiririka mashavuni mwao, na miili yao iliyoinama, yeye aliwaangalia kama watu wa Mungu. Hakuwaangalia kama watumwa. Yeye aliwaangalia kama watu wa Mungu waliochaguliwa.

⁵⁸ Na, loo, ninapoenda kote, nchi hadi nchi, na taifa hadi taifa, nikihubiri! Tangu nilipoiacha milango ya maskani hii, ambayo ni shirika lisilobagua madhehebu, lisilo na sheria ila upendo, halina kitabu ila Biblia, na halina kanuni ya imani ila Kristo, nimejaribu kuwaangalia watoto wa Mungu, na juu ya waliokataliwa, kuwa ni watu wa Mungu waliochaguliwa na

kuteuliwa. Siwaulizi kama wao ni washiriki wa Maskani ya Branham. Siwaulizi kama wao ni Methodisti, ama kama wao ni Wapresbiteri, ama kama wao ni Wapentekoste, ama Wanazarayo, ama Pilgrim Holiness. Ninataka kuwaangalia tu kama watu wa Mungu. Nami nikiyaona matendo yao na kazi yao, kwamba ni watumishi wa Bwana Mungu. Nao moyo wangu una shauku ya kushiriki pamoja nao, haidhuru wana chapa gani. Ninatamani tu ushirika wao. Ninawapenda kwa sababu ninajua wao ni watu wa Mungu.

⁵⁹ Ninapomwona mwanamke akishuka mtaani, amevaa sketi ndefu, na nywele zake zimetengenezwa vizuri huku nyuma, na—na amevaa gauni linaloonekana la heshima; kisha ninamwona msichana mwingine, labda umri uo huo, amevaa maskini kaptura; huenda akawa, kwa sura, mrembo mara mbili ya huyo mwanamke mwenye nywele ndefu, kulingana na mtazamo wa ulimwengu, lakini nitasimama na msichana huyo aliyevalia kama Mkristo. Ingawa watakuwa wakimcheka, na kumwita mlokole, hata hivyo, nitachukua msimamo wangu. Huenda asiwe mrembo kama huyo msichana mwingine, kimaumbile, lakini yeye anaona kitu fulani. Kwa imani anamwona Yeye Yule asiyeonekana, Ambaye anayaongoza maisha yake.

⁶⁰ Ninapomwona mtu kwenye wajibu wake, akiitwa “shemasi,” ama “mhubiri,” ama “mlokole,” kwa sababu anakataa kuvuta sigara, na kunywa pombe, na kwenda kwenye madansi, kama hao wengine, naye anaitwa “mlokole,” moyo wangu unavutiwa naye. Yeye ni ndugu yangu, huku katika udongo huu wa Misri, hilo linaufanya moyo wetu uwe na shauku ya kumkumbatia na kusema, “Ndugu, sisi ni wasafiri na wageni, wa nchi hii, nami nina shauku ya kushiriki nawe.”

Ilimbidi Musa kujichagulia, kuchagua kwa imani.

⁶¹ Ni vijana wanaume wangapi wangaliirukia nafasi hiyo ya kuwa mwana wa binti ya Farao! Ni vijana wanaume wangapi wangeirukia nafasi hiyo ambayo Musa alikuwa nayo, kuzifurahia anasa zote na madoido ya ulimwengu, wapate kuwa mfalme wa Misri, kuwa na ulimwengu mzima chini ya miguu yake! “Ni jambo la kijinga jinsi gani,” ambalo vijana wanaume wa siku zake hapana shaka waliwazia, “wakati Musa alipochagua kupachukua mahali pake na watu wa Mungu wanaoteseka na kudharauliwa.”

⁶² Kwa nini akafanya jambo hilo? Kwa imani, hapo alipoyainua macho yake, aliangalia kupita madoido ya ulimwengu huu. Yeye aliangalia kupita hizo anasa za dhambi. Nayo Biblia ilisema ya kwamba yeye alistahimili kama amwonaye Yeye Yule asiyeonekana, kwa imani, ndipo akachagua kumtumikia Mungu huyo haidhuru ni jambo gani lililotukia.

⁶³ Halijabadilika. Wengi wetu wangeweza kwenda kwenye lile tungaliliita jengo bora zaidi. Tungeweza kufurahia, labda,

ushirika na anasa za kuketi kwenye benchi bora zaidi. Huenda tukawa maarufu zaidi, kunywa pombe na kuvuta sigara, na kuvalia na kutenda kama ulimwengu. Lakini kuna shida gani? Umeyainua macho yako, na kwa imani ukamwona Yeye Yule asiyeonekana, na umechukua msimamo wako pamoja na waliokataliwa na wanaoitwa watakatifu wanaojibingirisha wa siku hizi. Kwa kuwa kwa imani tunamwona Yeye Yule asiyeonekana, tukichagua maudhi na mateso.

⁶⁴ Nisingewaambia watu kwamba wanapaswa kuchagua kuteswa. Sisemi kwamba mnapaswa kuchagua mateso. Hilo lisingekuwa ndilo jambo la kibinadamu kufanya. Lakini kama kuteseka kuko kwenye njia ya jukumu lako, basi hebu na tukabiliane nako vile kunavyokuja. Sitaki ufanye jambo fulani ili mtu fulani akudhihaki. Nisingekutaka useme mambo tofauti, ya kwamba, “Mimi . . . mimi ni mfuasi wa kanisa ambalo haliadini *hili-na-hili*, ulimwenguni,” na mambo kama hayo, kuwafanya tu watu wakudhihaki. Unajiletea hayo mwenyewe. Nisingekwambia utoke hapa nje na kupiga makelele na kufanya kitu ambacho kilikuwa ni cha msimamo mkali. Nisingekutaka ufanye hivyo, kusudi mtu fulani aseme kwamba wewe ni mlokole. Unajiletea hilo mwenyewe. Lakini ikiwa kwenye njia ya jukumu lako kwa Mungu, acha walimwengu waseme wanalotaka kusema. Wewe endelea kuishi.

Unafanya chaguo. Kila mwanamume na mwanamke hana budi kufanya hili.

⁶⁵ Vipi kama Farao angalionga yale Musa aliyoon? Yeye aliyaona mateso ya hao watu. Alijua gharama aliyokuwa aliye. Bali kwa imani alichagua hayo, kuliko kupata anasa za dhambi.

⁶⁶ Kunao labda maskini wasichana wadogo, wanaoketi hapa, kama wasichana wadogo wanaomeremeta. Ulimwengu ungetaka kuwaambia, “Fanya *hivi-na-hivi*. Wewe ni mrembo. Mwili wako umeumbwa kirembo sana. Inakupasa kuanika huo.”

⁶⁷ Lakini, dada yangu, inua macho yako na kuangalia kupita hayo, kwake Yeye aliyesema, “Ni chukizo kwa mwanamke kuvaa mavazi yampasayo mwanamume.”

⁶⁸ Kama wanaume wa watu katika jamii yako, kama wanawake unaoshirikiana nao, walisema, “Ikate hiyo nywele ndefu. Ingekuwa ni baridi kidogo. Ingekuwa *hivi, vile*, ama *vinginevyo*.” Ama, “Ingekufanya bora zaidi.” Usisikilize hilo!

⁶⁹ Wewe inua macho yako, na kwa imani umwone Yeye aliyesema, “Nywele za mwanamke ndizo fahari yake, naye hatazikata.”

⁷⁰ Kama wakisema, “Lingekuwa maarufu. Utasimama vema zaidi kazini mwako, ama kwa bosu wako, kama ukinywa kileo. Kama ungevuta sigara kama hao wanawake wengine, ungetambulika vizuri zaidi katika ujirani wako.”

⁷¹ Kwa imani yainue macho yako umwangelie Yeye Yule aliyesema, “Utie mwili huu najisi, nami nitauangamiza.” Kwa imani tunayaamini mambo hayo. Sio kitu ulichokiona. Ni kitu unachokiamini. Kwa imani, Musa alifanya.

⁷² Na katika safari hii ya imani, unakuja wakati hapana budi pawe na chaguo.

⁷³ Lutu alifanya kosa hilo la kusikitisha tunalolifanya. Mara nyingi tunachagua kwa wema wetu wenyewe. Tunachagua vitu ambavyo vingekuwa bora zaidi.

⁷⁴ Wakati mwingine kukitokea ugomvi kidogo kanisani, halafu mtu fulani aseme, “Vema, shemasi ama mchungaji yuko upande huu.” Usiangelie hilo. Angalia kilicho haki. Ondoa kitu hicho na uwapatanishe. Huo ndio utauwa.

⁷⁵ Kunalo chaguo. Nasi tunajichagulia. Tunachagua kitu ambacho ni cha manufaa kwetu.

⁷⁶ Lakini Musa alichagua mateso na dhihaka, apate kutembea pamoja na watu wa Mungu. Wazia jambo hilo sasa. Lisikilizeni. “Alichagua mateso ya watu wa Mungu, na kuyahesabu hazina kuu zaidi, kwa kuwa alistahimili, akimwona Yeye Yule asiyeonekana.”

Sasa, Lutu, wakati mmoja, ilibidi afanye chaguo.

⁷⁷ Na huenda ikawa, asubuhi ya leo, kwamba kutakuwako na wanaume na wanawake walioketi hapa, mtakaofanya chaguo lenu la mwisho. Wewe leo uko jinsi ulivyo, kwa sababu miaka kadhaa iliyopita ulichagua kuwa kile ulicho sasa. Halafu kile unachochagua sasa kitaamua kile utakachokuwa miaka mitano kuanzia leo. Miaka mitano kuanzia leo huenda ukawa mmishenari. Miaka mitano kuanzia leo huenda ukawa Mkristo mashuhuri.

⁷⁸ Ama, miaka mitano kuanzia leo huenda ukawa katika kuzimu, kwa sababu ulifanya uamuzi mbaya. Miaka mitano kuanzia leo huenda utakuwa ukisafisha mahali pa kutemea mate kwenye baa. Miaka mitano kuanzia leo huenda ukawa kahaba mtaani.

⁷⁹ Ama, huenda ukawa ni mwanamume ama mwanamke ambaye—ambaye ana sifa njema kwa jamii yoyote, kwa sababu ya chaguo lako la Kristo. Miaka mitano kuanzia leo huenda ukawa Utukufuni, umeondoka katika Unyakuo, kwa sababu ulifanya chaguo leo.

⁸⁰ Lakini huna budi kuchagua. Na usiangelie unayoona. Chagua yale unayoona kwa imani. Hicho ndicho kitu pekee kitakachojalisha, ni kile unachochagua kwa imani.

⁸¹ Lutu, kwa kuwa ilimbidi kufanya chaguo. Ibrahimu alimpa Lutu chaguo lake.

⁸² Naye Mungu hukupa chaguo lako. “Chagueni hivi leo yule mtakayemtumikia.” Katika bustani ya Edeni kulikuwako na mti wa—wa maarifa, na Mti wa Uzima. Mwanadamu alipewa majaliwa ya kuchagua wowote aliopenda. Na ndivyo ilivyo leo. Unapewa majaliwa yako, kama wenye hiari ya kujichagulia, kuchagua chochote unachotaka kuchagua.

⁸³ Ushauri wangu kwako, ni, usiangalie mambo ya kisasa yanayokuzunguka, na umaarufu na uvutio ambao wewe ungeweza kuwa nao. Bali chagua, hasa, kwa imani, Yeye aliyeitoa hiyo ahadi ya kwamba siku moja Yeye atakuja na kusahihisha makosa yote, kisha atakupa Uzima wa Milele, na kufufua. Haijalishi kama utachukua njia iliyodharauliwa pamoja na wachache wa Bwana, fanya chaguo hilo. Kukiweko na matatizo karibu nawe, kukiweko na matatizo nchini, kukiweko na matatizo kanisani, kukiweko na matatizo nyumbani, haijalishi yalipo, fanya chaguo lako, “Kwa imani, nitamtumikia Mungu. Nitaunyenyekeza moyo wangu Mbele Zake. Nitashika njia pamoja na watoto wa Mungu. Ninawaona wamedharauliwa na kukataliwa, na kusukumwa nje na kudhihakiwa, bali ningali nitashika jukumu langu. Nitakaa karibu tu. Ndipo wakati watakapolia, nitalia pamoja nao. Na wakati kukiwako na huzuni, nitahuzunika pamoja nao. Jinsi wanavyoishi, nitaishi.”

⁸⁴ Kama vile Naomi alivyosema... Ama, Ruthu alivyomwambia Naomi, “Njia zako ziwe njia zangu. Njia zangu ziwe njia zako. Mahali unapoishi, nitaishi. Uendako, nitaenda. Mungu unayemtumikia atakuwa ndiye Mungu wangu.” Fanya chaguo hilo, hata ikichuna ngozi yenyewe ya dhamira yako, ya kufikiria kwamba wewe ni mtu mashuhuri. Jichune ngozi kabisa na ushike njia pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, na ukae mwaminifu kwenye huduma ya utumishi na kwenye jukumu lako.

⁸⁵ Lutu aliangalia kila mahali. Akasema, “Ninalo chaguo.” Naye akaelekeza macho yake Sodoma. Akaona mbuga zilizojaa nyasi zilizokuwa nzuri kushinda zile Ibrahimu alizoon, na mahali Ibrahimu alipokuwa. Aliona nafasi ya kuwalisha ng’ombe wake, awe na ng’ombe wanono na bora zaidi.

⁸⁶ Ninatumaini siudhi hisia ya mtu yeyote. Lakini huo umekuwa ndio msimamo wa wahubiri wengi kupita kiasi, kupatana pamoja na Injili, wakidhania ya kwamba wanapata fedha nyingi zaidi kutoka kwake. [Ndugu Branham anapiga makofi mara tatu—Mh.] Tikiti ya posho! Afadhali niishi katika nchi kavu, nile, ninywe maji kutoka kwenye tawi, na kula biskuti kavu, kuliko kupatana juu ya imani yangu katika Neno la Mungu aliye hai. Nitashika njia yangu.

⁸⁷ Baadhi yao walisema, “Billy, mkutano wako una shida gani, kwa kuwa kuna Wapentekoste wengi kupita kiasi mle.” Mhudumu mashuhuri sana wa kimadhehebu alisema hivyo.

Nikasema, “Hivi dhehebu lako litaudhamini mkutano wangu?”

⁸⁸ Sio muda mrefu uliopita, katika gazeti la *Look*, ninaamini, kulikuwako na makala. Naye mwandishi akasema pale, akazungumza kuhusu Wapentekoste. Akasema, “Kanisa la Kipentekoste ndilo kanisa linalopanuka upesi kuliko yote ulimwenguni siku hizi.” Kwa nini? Ni kwa sababu wanaume na wanawake wameyainua macho yao na kuangalia mbali sana.

⁸⁹ Naye huyo mwandishi pia akawapongeza Wapentekoste. Loo, hakika, yeye alisema, “Kulikuwako na baadhi yao walioshika msimamo mkali, na kadhalika. Lakini, Methodisti inaabudu kanuni ya imani. Wanamwabudu Mungu kwa kanuni ya imani. Baptisti inafanya vivyo hivyo, na Wapresbiteri. Lakini Mpentekoste huabudu kwa Biblia yake.”

⁹⁰ Kwa imani tunaiona ile ahadi. Nitachukua msimamo wangu pamoja nao, haidhuru wanadharauliwa jinsi gani, mimi ningali ni mmoja wao. Ingawa huenda wakadhihakiwa, na kuwa na mema na mabaya yao, kama vile Israeli walivyofanya, kamwe sitapenda kusimama na manabii wa uongo kando ya kilima, Balaamu, na kujaribu kulaani kile Mungu amebariki. Kwa sababu, kwenye kambi hiyo mna Mwamba uliopigwa, na Dhabihu iliyolowa damu, na Nguzo ya Moto. Haijalishi wako katika kitu gani, kinawaongoza kwenye ushindi, nao hawana budi kuufikia, kwa sababu wao ni watu walioahidiwa wanaotembea kwa imani. Ingawa wao si dhehebu, walikuwa ni wazururaji kote, na ndivyo walivyo watu wa Mungu. Lakini ninataka kushika njia yangu pamoja nao, nijiunge nao katika viwango vyao; si katika dehebu lao, bali katika ushirika wao katika mambo ya Roho wa Milele wa Mungu, ambapo, kwa imani nimepokea ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mungu na anisaidie daima kuwa na msimamo huo.

⁹¹ Angalieni. Wakati wakiendelea, tunaona ya kwamba Lutu aliona nafasi nyingi za kupata ng’o—ng’ombe wanono. Wengi wanaona nafasi nyingi za pochi nono. Wengi huona nafasi za hadhi bora ya kijamii. Aliona uwezekano wa dola chache za ziada. Aliona uwezekano wa kuwa meya wa mji. Akiwa ni mgeni, na mtu mwerevu sana, kama alivyokuwa, “Labda nitakuwa mtu mkubwa sana wa mjini.” Aliona uwezekano kwa sababu zilikuwa zimewekwa mbele zake. Lakini hakuona ule moto uliokuwa uangamize nchi. Yeye hakuridhika, kwamba hiyo nchi ilikuwa imejaa dhambi, na ilimbidi Mungu kuiangamiza.

⁹² Na, leo hii, watu hujaribu kujiridhisha kwa kusema, “Hivi wewe...?”

Nitasema, “Je, wewe ni Mkristo?”

⁹³ Wanasema, “Mimi ni Mmarekani.” Hilo halina uhusiano nalo zaidi ya kujaribu kumwambia kunguru kwamba alikuwa ni

chura. Halina uhusiano wowote nalo. [Ndugu Branham anapiga makofi mara moja—Mh.]

⁹⁴ Itaangamizwa, kwa sababu Mungu ni mwenye haki. Na kama Marekani ikipita na dhambi zake, Mungu mtakatifu, aliye mkuu na mwenye haki atawajibika ku—kuifufua Sodoma na Gomora na kuwaomba msamaha kwa kuwateketeza, kwa sababu ya dhambi yao; kama akituacha tupite nayo.

⁹⁵ Kama akikuruhusu kuingia Mbinguni kwa kazi zako mbovu, itambidi Yeye kumfufua Anania na Safira na kuwapa nafasi nyingine. Hakika angefanya hivyo. Lakini Yeye ni mwenye haki. Anania aliona fedha zake. Petro akamwona Kristo.

⁹⁶ Loo, jamani! Lutu hakuona maangamizi ya watoto wake mahali pale.

⁹⁷ Wengi wenu, siku hizi, mnaoshikilia karibu na maskini kanuni hizi za imani na kadhalika, hamwoni ule uhalifu wa vijana na maangamizi ya watoto wenu. Humwoni binti yako katika nyumba ya ukahaba. Humwoni mwanao mlevi, ama kwenye meza ya karata mahali fulani.

⁹⁸ “Kwa sababu yeye ana maji tele.” Na dhambi haiguswi. Hakumwona mke wake, mkubwa wa mashirika yote, akigeuka kuwa nguzo ya chumvi, wakati akiangalia. Hakumwona akiponea chupuchupu, kwenye mji mdogo mahali fulani, kuyaokoa maisha yake. Hakuona hilo, kwa sababu alitazama tu alichoon a mbele zake.

⁹⁹ Lakini, Ibrahimu, hakuitazama hiyo nchi yenye maji tele, kwa kuwa aliyainua macho yake akaona kesho, kwa kuwa yeye angerithi vitu vyote. Mkristo halisi leo hii huinua macho yake na kuona ahadi ya Kristo: “Heri wenye upole kwa kuwa watarithi vitu vyote. Watairithi nchi.” Mkristo halisi, kwa imani, huangalia juu na kuona hayo. Mwrite utakalo. Yeye aliinua macho yake. Ndipo wakati alipofanya hivyo, Mungu alisema, “Ibrahimu, tembea kote katika nchi, yote ni yako.” Kwa imani, Ibrahimu alifanya jambo hili; imani ile ile aliyokuwa nayo Musa.

¹⁰⁰ Iliandikwa na mfafanuzi mmoja, aliyesema haya. Nilifikiri yalikuwa ndiyo maneno ya kupendeza kuliko yote. Kwamba Ibra-... “Musa aliyachukua mambo ya ulimwengu yaliyo bora kuliko yote na kuyaweka kwenye mizani; na mambo ya dini yaliyo mabaya kuliko yote, akayaweka kwenye mizani; ndipo mambo ya dini yaliyo mabaya kuliko yote yakayashinda mambo ya ulimwengu yaliyo bora kuliko yote.”

¹⁰¹ Ndivyo ilivyo siku hizi, ya kwamba kama tukitwa chochote tunachotaka kuitwa, “walokole,” ama “waponyaji wa Kiungu,” ama “mtakatifu anayejibingirisha,” ama chochote wanachotaka kutuita. Kibaya kuliko vyote tulicho kitashinda kilicho kizuri kuliko vyote ulimwengu unachoweza kutoa. Hutaki kuitwa “wa mtindo wa kale, mzee mjinga, mlokole.” Itashinda kilicho bora kuliko vyote ibilisi alich nacho cha kukupa. Hakika itashinda.

¹⁰² Musa alihesabu kushutumiwa kwa Kristo. Alimwona Kristo kimbele. Baadaye alinena baadhi ya maneno ya kuvutia sana kumhusu Yeye. “Mnaona, Bwana Mungu wako atakuondokeshea nabii kama nilivyo mimi.” Yeye alijua. Alitangulia kumwona, naye akahesabu kushutumiwa Kwake kuwa ni utajiri mkuu kuliko madoido ya ulimwengu.

¹⁰³ Rafiki Mkristo, leo hii, hivi huwezi kufanya hivyo? Na madoido yote na kupendwa sana na watu wa ulimwengu, kwa imani, tunamwona Yeye aliyeahidi. Na yaliyo mabaya kuliko yote ya kanisa siku hizi, katika hali yake yote, hata hivyo Hayo yatashinda kila kitu ibilisi anachoweza kukupa. Kama tumevurugika, kama tumevunjika vipandevipande, kama tumechanganyikiwa na kutengana, katika madhehebu na ulokole, itashinda chochote ibilisi anachoweza kukupa. Bila shaka.

¹⁰⁴ Yeye alikuhesabu kushutumiwa kwa Kristo kuwa ni utajiri mkuu kuliko hazina zote za Misri. Ndipo ikambidi kufanya jambo fulani. Akaacha Misri. Loo, ninalipenda neno hilo. Akaacha Misri. Mnaona, alikuwa akiangalia kupitia dirisha lile lile, bali alikuwa akiangalia tofauti na Farao. Vipi kama Farao angaliuona mwisho wake? Vipi kama Farao angaliliona taifa lake likizamishwa? Musa aliliona. Vipi? Kwa sayansi? Kwa imani, Musa aliliona. Kila kitu alichofanya kilikuwa ni kwa imani, kwa sababu Mungu alimwahidi Ibrahimu, baba yake, kwamba Yeye ange—Yeye angelizuru taifa hili baada ya miaka mia nne, naye angewatoa. Basi kwa imani, Musa aliamini Neno ambalo Mungu alisema, naye akajua mwenyewe, kama kwa imani, alikuwa kiongozi aliyechaguliwa kuwatoa. Yeye alijua mahali alipokuwa. Alichukua mahali pake kwenye yale mashimo ya kinamasi, kama mkanyaga matope, na kuhesabu kushutumiwa kwa Kristo kuwa ni utajiri mkubwa kuliko kuketi kwenye kiti cha enzi cha Misri. Alichukua . . . Kamwe yeye hakusema, “Ninawahurumia.” Alichukua mahali pao na kuambatana nao! Utukufu kwa . . . Alipachukua mahali pao. Tuliambatana nao.

¹⁰⁵ Si ajabu yule mwandishi aliyevuviwa alisema:

Nitashika njia na wachache wa Bwana waliodharauliwa.

Nimeanza pamoja na Yesu, sasa ninapita.

Niko njiani nikienda zangu kwenye nchi ya Kanaani. (Hakika.)

¹⁰⁶ Musa. Ilisemwa na mtu mmoja kwamba afadhali Musa, wakati yeye angalikuwa mwana wa Farao na alikuwa na urembo wa ulimwengu, afadhali awe mwana wa Ibrahimu kuliko kuwa mwana wa Farao. Mwana wa Ibrahimu, aliyedharauliwa, kuliko kuwa mwana wa Farao, mfalme.

¹⁰⁷ Afadhali niwe mwana wa Bwana Yesu, na mtumishi mwenzake, na kupachukua mahali pangu pamoja na watu

wa ulimwengu huu waliokataliwa, kuliko kuwa Rais wa hii Marekani kuu, ama kuwa Elvis Presley, ama Pat Boone, ama yeyote unayetaka kumfanya. Nitaichukua njia yangu.

¹⁰⁸ Wasichana wanapaswa kuichukua njia yao. Badala ya kuwa Ma—Mary Pickford, ama bingwa fulani mashuhuri wa sinema, msichana fulani mwenye ubembe, shika njia yako pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa.

¹⁰⁹ Afadhali niwe mhubiri mimbarani, nikihubiri utajiri wa Kristo usiotafutika, kuliko kuwa bingwa wa sinema wa Hollywood, ama mtu aliye mashuhuri kuliko wote duniani. Kama ilinibidi kula haba, kuombaomba, ama chochote kilichonilazimu kufanya, nitashika njia na watu wa Bwana. Kwa imani, ninafanya hivyo. Nimepewa nafasi nyingi. Lakini, kwa neema ya Mungu, ningali ninaona kwa imani.

Kwa imani ninaweza kuiona kwa mbali;
Naye Baba yetu anangojea njiani,
Kutuandalia makazi Kule.

¹¹⁰ Mtu mmoja wa kodi ya mapato alisema, hivi majuzi, “Kwa nini ukaiweka nyumba yako rehani kwa kanisa hilo? Kwa nini kutoa nyumba yenye gharama ya dola elfu ishirini na tano kwa maskini ile maskani inayoonekana kama takataka?”

¹¹¹ Nikasema, “Sikufanya hivyo kwa kanisa. Ni kwa hao watu walio huko.” Sina yoyote ya mali ya dunia hii. Kila hela ya pesa nilizowahi kuchukua imerudishwa kwa kanisa hili. Kwa nini? Imani yangu iko katika Mungu, na si katika mambo ya ulimwengu huu. Upendo wangu uko juu. Nami ninaamini nyote ndivyo mlivyo, kama mko sawa na Mungu. Ni kweli, kwamba ndivyo mlivyo. Sisi, kwa imani, tunapokea. Sisi, kwa imani, tunamwamini Mungu.

¹¹² Musa, ilimbidi kufanya chaguo. Ndipo basi ilimbidi, baada ya kufanya chaguo, ilimbidi kuipigania imani, wakati huo, kwa kuwa hakuigopa ghadhabu ya mfalme. Sasa, kibinadamu, yeye alikuwa na haki ya kuiigopa ghadhabu hiyo. Alikuwa na haki ya kuiigopa ghadhabu ya mfalme, bali hakuigopa. Hakufanya hivyo, kwa sababu alikuwa na kazi ya kufanya, naye alikuwa kwenye jukumu lake. Wala hakujali yale mfalme aliyosema kulihusu. Alishika njia yake vile vile tu.

¹¹³ Sasa, Farao, hakika, wakati anapoona ameshindwa, yeye alitaka kumpa Musa na wale watoto... Akasema, “Vema, nitakwambia yale nitakayofanya. Ninyi nyote kaeni tu nchini na mtoke mwende mkamtolee Mungu wenu dhabihu.”

¹¹⁴ Hivyo ndivyo ibilisi anavyofanya kazi. “Loo, mnaweza kuwa wa kidini. Kwa nini msiende na kujiunga na kanisa fulani? Haiwabidi kufanya mambo haya yote.” Mtu anamwambia mkewe...

¹¹⁵ Mke anasema, “Mume wangu, niliokoka. Hakuna tena rangi ya makucha, ama rangi ya midomo na kadhalika. Hakuna haya tena. Hakuna karamu tena. Hakuna mambo haya ya vyama vya kijamii tena. Nimeachana nayo! Nitaweka wakati wangu katika kulisoma Neno, kuishughulikia nyumba.”

¹¹⁶ “Sasa, angalia, mpenzi. Wewe, unaweza kuwa wa kidini, sawa. Sasa, angalia, wewe—wewe nenda *huku*. Una kanisa baya.”

¹¹⁷ La, hapana. Uko katika la kweli. Kama una mhubiri atakayekuhubiria hayo, unapaswa kukaa nayo. Tafuta kote katika Maandiko uone kama hiyo ni kweli.

¹¹⁸ “Loo,” kasema, “nenda *huku*. Haiwabidi—haiwabidi kufanya hayo huku. Mnaona? Hawafanyi hivi huku.” Hivyo ndivyo... “Nenda tu umbali huo.” Bali yeye hawataki mtoke nchini. Hivyo ndivyo ibilisi afanyavyo. Yeye hataki mtoke kwenye mambo ya ulimwenguni; kuingiza tu ulimwengu pamoja na kanisa.

¹¹⁹ Hivi majuzi, nikishuka kuja barabarani, niliifungua redio yangu. Na kulikuwako na wi—wimbo, nami nikaendelea kusikiliza, ndipo ikanibidi kuchukua, karibu, wimbo wote, kabla sijaweza kujua kama ulikuwa kabisa ni wimbo wa kidini, ama ibilisi akijaribu kuyashusha mambo ya Mungu kufikia kiwango cha ulimwengu. Huwezi kufanya hilo! Mungu turehemu!

¹²⁰ Sijali ni alamu ngapi Elvis Presley ataandika, za nyimbo zote nzuri za kidini. Angali amepagawa na pepo. Yeye aliwatuma watoto wengi zaidi kuzimuni, na shughuli zote nijuazo, ulimwenguni kote siku hizi. Pat Boone na hao wengine, yeye alikuwa mfuasi wa church of Christ; na Elvis Presley, Mpentekoste; hao ni Yuda Iskariote, katika mfano wa watu hao. Ibilisi anajaribu kuleta mambo makubwa ya Mungu, kusudi waweze kuyachanganya hapa *chini*. Watu hawataangalia juu ya *hili*. Wanaangalia tu *hapa*, kasema, “Vema, yote ni sawa.” Si sawa. Ondokeni kwenye hiyo nchi.

¹²¹ Kasema, “Mnaweza kwenda siku chache tu. Nanyi nendeni, mkakae nchini.” Hakika, yeye alijua wangerudi. Ndipo akakuta kwamba hilo lisingefanikiwa, kwa hiyo akawazia jambo lingine. Akasema, “Nitawaambia la kufanya. Nyinyi nendeni popote mnakotaka kwenda, bali muwaache wake zenu wote, watoto wenu wote, na ng’ombe wenu wote, *huku*. Waacheni hapa, nanyi mwende.” Maana, yeye alijua walikuwa na mali huko nyuma, ambayo ingewashawishi kurudi.

¹²² Na hivyo ndivyo ibilisi anavyokwambia. Mradi tu unaacha baadhi ya mambo ya ulimwengu yakining’inia juu yako, ungali unataka kuvuta sigara, unataka kunywa pombe, unataka kuvalia kama walimwengu, hivyo ndivyo ibilisi anavyotaka.

123 Ninasikia mengi sana kuhusu kurudi nyuma. Siamini kuna kurudi nyuma kwingi kama vile watu wanavyodhania kunako. Wanaacha tu mali nyingi kupita kiasi Misri kuwashawishi warudi, hivyo tu. Kurudi nyuma si vile wanavyosema kulivyo. Uliacha mengi sana ya ulimwengu kule nyuma, ambayo yanakuvutia.

124 Ndugu, nakwambia, Israeli walipokuwa tayari, usiku wa manane, walikuwa na kila kitu walichokuwa nacho katika ulimwengu huu, kimepakiwa na tayari kuondoka.

125 Mungu na atutumie uamsho wa namna hiyo. Tuandae kila kitu, na tuwe tayari kuondoka. Kelele za usiku wa manane zinakuja, "Tokeni mwende kumlaki." Afadhali uwe umeandaa kila kitu. Afadhali msiwe na chochote, ulimwengu huu, kuwavuta nyuma, kamba zozote za kuwashikilia chini. Jitayarishe. Hebu tuwe tayari. Tunaondoka.

126 Nanyi mwajua nini? Nawaambia, walikuwa wakweli sana kwa Mungu, hata Farao akasisimkwa sana usiku wa manane, akasema, "Ondokeni! Ondokeni, mshike njia. Chukueni kila kitu mlichochacho, mwende!"

127 Nina furaha sana kwamba mtu anaweza kuishi karibu sana na Mungu, hata ibilisi asijue la kufanya naye. Hiyo ni kweli. Ondokeni! Shikeni njia! Mtiini Mungu!

128 Kwa imani, yeye aliiona ile ahadi. Wakanyaga matope, ama si wakanyaga matope, alichukua njia yake na wachache wa Bwana waliodharauliwa. Farao akasema, "Chukueni yote mliyo nayo mwondoke hapa! Sijui la kufanya na nyinyi." Yeye alikuwa mkweli sana kwa Mungu, kwa imani.

129 Imani itafanya miujiza, ikiwa utadumu mwaminifu kwa Mungu. Kwa imani, tunamwona Yeye.

Wakati wetu umekwisha; tumepitisha wakati.

130 Bali, kwa imani, asubuhi ya leo, inueni macho yenu. Msiangalie yaliyo karibu nanyi, ulimwengu huu wa kisasa, bali tazameni mkamuone Yeye Yule aliyetoa ahadi. Biblia ilisema, "Hatuoni mambo yote kikamilifu sasa, bali tunamwona Yesu." Mwangelieni Yeye, asubuhi ya leo, nazo njia zenu zitabadilika.

131 Tunapoviinamisha vichwa vyetu, kwa muda kidogo tu, kwa ajili ya maombi. Bwana na aongeze baraka Zake kwenye Ujumbe.

132 Wazia moyoni mwako sasa. Hivi umekuwa ukiviangalia vitu vya ulimwengu? Kwa imani, unamwona Yesu? Unaangalia umaarufu wako, kanisa lako? Msimamo wako wa kijamii ulivyo na walimwengu? Ama, unamwona Yesu Ambaye, katika huruma, alijiweka Mwenyewe kwenye mkono wa kulia wa Ukuu huko Juu, Ambaye aliteswa kama mfia imani, mwenye haki kwa wasio haki? Hivi huwezi kuyainua macho yako na kuuona ule Mti wa

Uzima huko ng'ambo? Basi, achana na mti huu wa sayansi na maarifa, ukamtumikie Yeye.

¹³³ Ungetaka kukumbukwa katika maombi kabla sijaomba? Inueni mikono yenu, kwa ajili ya haja yoyote ambayo huenda unahitaji. Mungu awabariki. Anaona mkono wenu nyote.

¹³⁴ Kama wewe ni mwenye dhambi, inua macho yako na utazame sasa. Kama umekuwa asiyejali, kama umekuwa na ugomvi mdogo na vitu vidogovidogo, inaleta tofauti gani? Utakufa moja ya siku hizi. Siku gani? Labda leo! Hujui. Saa moja kuanzia sasa, huenda ukawa kuzimuni, ama huenda ukawa Mbinguni. Lakini huna budi kuchagua sasa. Kama kuna kitu chochote maishani mwako ambacho si sahihi, wewe chagua sasa, kwa imani.

¹³⁵ Unasema, "Vema, laiti ningeweza kujilipizia kisasi kwa huyo mama! Laiti ningeweza kujilipizia kisasi kwa huyo mwanamume!" Haijalishi walifanya nini, chagua Uzima. Chagua Uzima.

¹³⁶ Kwa kuwa, Yesu alisema, "Kama kutoka moyoni mwako hutamsamehe kila mtu makosa yao, wala Baba yenu aliye Mbinguni hatakusamehe." Kwa hiyo kuwa tu karibu hivyo. Kukiwapo na kitu kimoja moyoni mwako dhidi ya mtu yeyote, mwenye dhambi au mtakatifu, uko kwenye hatari ya moto wa jahanamu.

¹³⁷ Sasa inua macho yako. Unaona nini, adui yako? Ama, unamwona Mwokozi wako? Unatazama nini asubuhi ya leo?

¹³⁸ Ikiwa wewe ni mgonjwa, naye daktari wako anasema ya kwamba huwezi kupona, inua macho yako, msalabani, ambapo Yeye alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo Yake tuliponywa. Usiangalie yale daktari asemayo; yeye anafanya kazi katika sayansi. Imani hufanya kazi katika milki ya Roho na Mungu. Hebu tuwazie mambo haya sasa wakati mmeinua mikono yenu. Mungu ameiona.

Na tuombe.

¹³⁹ Ee Mungu wa Milele, katika utulivu wa ibada hii sasa, baada ya Ujumbe kutolewa, usiache mbegu hizo za Neno Lako, Bwana, zianguke penye mwamba. Usiuache huu Ujumbe, Bwana, uanguke penye michongoma, miiba, hata shughuli za maisha haya (kama ya Lutu) ziweze kuusonga, hatimaye, uwe umekatiliwa mbali. Lakini, Ee Mungu mbarikiwa, jalia uanguke penye udongo mzuri, wenye rutuba, kwenye mioyo iliyotubu. Na juu ya wangu, pia, Bwana, ili sote tuweze kuangalia kupitia kioo cha Mungu cha kuangalilia, na kuona Kanisa la Bwana Yesu lililokataliwa, watu waliokataliwa, njia iliyokataliwa, na jalia tutembe katika njia hii tukufu.

¹⁴⁰ Kama vile Musa, yeye hakujua mahali alipokuwa akienda. Hao watu hawakujua mahali walipokuwa wakienda. Hawakujua njia ya kupitia. Walianza tu.

¹⁴¹ Na, Ee Bwana Mungu, wakati wimbo huu mzuri unapochezwa, kwa imani tunaweza kuiona Nchi hiyo kwa mbali. Jalia iwe ni hivi sasa tu, kwamba wanaume na wanawake humu ndani hawatawazia yale ulimwengu utakayosema, wala vile wanavyoenenda. Jalia wainuke tu katika roho yao, waende.

¹⁴² Musa aliifuata ile Nuru, Nayo ikamwongoza hadi kwenye nchi ya ahadi. Bila kujua mahali alipokuwa akienda, bali alitembea tu katika Nuru, hadi kwenye ile nchi iliyokuwa nzuri kuliko mchana.

¹⁴³ Tujalie, Bwana, leo hii, kwamba wengi hapa waweze kutembea katika Nuru ya Maandiko na katika ushirika wa Roho Mtakatifu, na pamoja na Kanisa; Kanisa, Mzaliwa wa kwanza, watoto wachanga waliozaliwa upya ambao wamempokea Kristo, na wamejazwa na Roho Mtakatifu, wanaongozwa na Roho. Jalia tutembea katika ushirika huu, pamoja, kwenye vitu vya Mungu, tukimtumikia Yeye katika ubatizo, katika utii wa kifo Chake, kuzikwa, na kufufuka. Jalia tumtumikie katika amri Yake, “Ngojeni Yerusalemu hata mtakapovikwa Uweza utokao Juu.” Jalia tumtumikie katika uponyaji wa Kiungu, tukiwaombea wagonjwa. Jalia tumtumikie katika ushirika, kumega mkate, kwa umoja wa moyo, ushirika kwenye Neno la Mungu. Jalia tumtumikie katika vitu Vyake vyote vya Kiungu, mpaka Nchi hiyo itakapoonekana kwa macho. Tujalie, Bwana. Yasikie maombi yetu, tunapoyakabidhi yote Kwako sasa, katika Jina la Bwana Yesu.

¹⁴⁴ Sasa huku vichwa vyetu vimeinamishwa, kwa utulivu, polepole, hebu tuimbe tu wimbo huu. Sasa huku ni kuabudu. Ujumbe umekwisha. Mtu yeyote asiondoke. Iweni tu kimya. Na tuabudu.

¹⁴⁵ Ujumbe ni wa kusahihisha. Wazia sasa yale umefanya, yale uliyopaswa kufanya, kile kilichokufanya kile ulicho leo hii. Kinachokufanya uhukumiwe, leo hii, ni kwa sababu ulifanya kitu fulani jana. Itakuwa nini kesho? Lisahihishe leo, nawe utakuwa huru kesho. Unaona? Huna budi kuchagua. Unawezaje kufanya jambo hilo? “Kwa imani, sasa ninaachilia kila kitu. Sasa naachilia, na siku moja ninaenda Huko.”

Mahali pa raha hivi karibuni,
Tutakutana kwenye ile ninii nzu- . . .

Mwabudu tu Bwana katika roho yako sasa.

Mahali pa raha hivi karibuni,
Tutakutana na Kanisa lile lililodharauliwa.
(Mazingira magumu, bali tutakutana siku moja.)

Kwa Baba yetu mkarimu wa huko juu,
Tutatoa heshima yetu ya sifa,
Kwa ajili ya karama tukufu ya upendo Wake,
Na baraka zinazoitukuza ninii yetu . . .

Pamoja na wachache wa Bwana waliodharauliwa, kwa imani, ninachagua.

Katika mahali pa raha (katika mahali pa raha)
hivi . . . (karibuni)
Tutakutana kwenye pwani ile nzuri; (hivi
karibuni)
Katika mahali pa raha (katika mahali pa raha)
hivi karibuni,
Tutakutana kwenye pwani ile nzuri.
Kuna Nchi ambayo ni . . .

Mwabudu Yeye tu. Huku ni kuabudu.

. . . imani ninaweza kuona,

Kwa imani ninafanya chaguo langu.

Loo, Baba anangojea . . .

¹⁴⁶ Nawaona wote wa Bwana huko Ng'ambo; Ndugu George, Ndugu Seward, watakatifu wote.

. . . sisi makao Kule. (Naam, Bwana!)

Mahali pa raha . . .

¹⁴⁷ Baba yake, Howard, Edward, marafiki wote wazee watakatifu walioishika ile Njia, huko nyuma, muda mrefu uliopita.

Katika mahali pa raha (Naam, Bwana!) hivi
karibuni (hivi karibuni),
Tutakutana kwenye ile pwani nzuri.
Tutaimba kwenye ile ninii nzu- . . . (Ee
Mungu!)
Nyimbo tamu za waliobarikiwa, (Utukufu kwa
Mungu!)
. . . haitaona huzuni tena,
Wala kuhema wapate baraka ya Mahali hapo
pa raha.
Katika mahali pa raha, mahali pa raha hivi . . .
(hivi karibuni)
Tutakutana kwenye ninii nzu- . . .



KWA IMANI, MUSA SWA58-0720M

(By Faith, Moses)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, uliotolewa hapo awali katika Kiingereza Jumapili asubuhi, Julai 20, 1958, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2021 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org